The Tanganyika Law Society

The Bar Association Of Tanzania Mainland

**TAARIFA KWA UMMA**

**SUALA LA MWANANCHI ALIYEDHANIWA KUWA WAKILI AMBAYE TAREHE 23 MEI 2023 ALIRIPOTIWA KUFANYA FUJO KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI – KISUTU – DAR ES SALAAM**

Chama cha Sheria Tanganyika (Tanganyika Law Society - TLS) kinapenda kutoa taarifa kwa Wanachama wake na umma wa Watanzania kuhusiana na tukio lililotokea tarehe 23 Mei 2023 katika eneo la Mahakama ya Hakimu Mkazi – Kisutu, Dar es Salaam. Katiko tukio hilo, vyombo vya habari vilitoa taarifa kuwa mtu aliyefahamika kwa jina la Baraka Mkama na ambaye alitambulishwa kama wakili alionekana akiwazuia askari Polisi wasiwatie nguvuni wateja wake baada ya kuachiwa huru na Mahakama.

Baada ya kupokea taarifa hizo, tarehe 24 Mei 2023, Baraza la uongozi la TLS lilifanya kikao cha dharura na kuamua kuteua Kamati Teule ya Uchunguzi ambayo ilipewa hadidu za rejea za kufanya uchunguzi wa haraka na wakitaalam wa tukio hilo, kisha kuujulisha uongozi wa TLS kwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. Kamati hiyo ya watu wa nne ikiongozwa na Mwenyekiti wa TLS Tawi la Ilala, ilianza kazi yake tarehe hiyo hiyo 24 Mei na kukamilisha taarifa yake jana tarehe 26 Mei 2023. Kamati ilifanikiwa kumhoji mhusika – Baraka Mkama; na kisha mazungumzo na Jeshi la Polisi, Uongozi wa Mahakama pamoja na baadhi ya Mawakili waliokuwa na taarifa za tukio hilo. Kamati pia ilipitia mfumo wa usajili wa Mawakili *(e-Wakili)* ili kujiridhisha kuhusu taarifa za Baraka Mkama. Katika mahojiano na kamati, Mkama alikiri kuwa yeye sio wakili ingawa amekuwa akifanya kazi kama wakili tangu mwaka 2019. Vilevile katika mashauri aliyokuwa anayasimamia akiigiza kama wakili, alikuwa akiwatoza wateja wake shs milioni 3 na kuendelea kwa kesi.

**Baada ya kupokea taarifa ya kamati, Baraza la Uongozi la TLS liliipitia na kuijadili, kwa hivyo, tunapenda kuwafahamisha Wanachama wote wa TLS, Wadau wa TLS na Umma wa Watanzania kwamba, TLS TUMEJIRIDHISHA PASIPO SHAKA KWAMBA MHUSIKA WA TUKIO HILO NDUGU BARAKA MKAMA SIO WAKILI NA SIO MWANACHAMA WA TANGANYIKA LAW SOCIETY.**

Kwa sababu hiyo, TLS itashirikiana na vyombo vya dola na vyombo vya utoaji haki ili kuhakikisha kuwa hatua stahiki za kisheria zinachukuliwa dhidi ya mhusika, pamoja na watu wengine kama yeye ili kukomesha tabia hii ambayo inaelekea kuenea maeneo mengi nchini.

Katika kufuatilia tukio hili, TLS imepata taarifa muhimu za ziada kuhusu mtandao wa watu wasiokuwa mawakili wanaofanya kazi za uwakili (Vishoka) hivyo imeongezea muda Kamati Teule ya Uchunguzi kuendelea kufuatilia mtandao huo na kuwasilisha taarifa zake za ziada ifikapo tarehe 31 Mei 2023. Vilevile, TLS imekamilisha kuunda kikosi kazi ***(Anti-Vishoka Taskforce)*** kitakachofanya kazi ya kudhibiti watu ambao hawastahili kufanya kazi za mawakili. Baraza la Uongozi la TLS linaomba ushirikiano toka kwa Wanachama wa TLS, Wadau wa TLS na Wananchi katika hizi juhudi za kutokomeza uhalifu huu.

TLS inawakumbusha wananchi na wadau wake wote kila wakati kuhakiki taarifa za watu wanaoruhusiwa kufanya kazi za mawakili kwa kutumia mfumo wa utambuzi wa wakili wa Mahakama yaani ***e-wakili***. TLS itahakikisha kuwa inalinda na kusimamia maslahi ya mawakili; itawalinda na kuwatetea wananchi dhidi ya vishoka; na kushirikiana na vyombo vya dola katika kudumisha hadhi, nidhamu na heshma ya Mawakili kama maafisa wa Mahakama wakati wote.

Imetolewa leo tarehe 27 Mei 2023 na Baraza la Uongozi la TLS

**Harold Giliard Sungusia**
**Rais Wa TLS – 2023/24**

Secretariat: Plot 391, Chato Street, Regent Estate, Off Ally Hassan Mwinyi Road, Near AAR Hospital , Morocco, **Postal Address**: P. O. Box 2148, Dar es Salaam, Tanzania, East Africa, Telephone: (255-22)2775313/ Fax: (255-22)2775314 **E-mail:** info@tls.or.tz, Website: www.tls.or.tz